
Madhumuni ya Kichunguzi hiki cha Uandishi cha lugha ya nyumbani au msingi ni kupata wazo la jumla la stadi za kuandika za Wanafunzi watarajiwa ambao Elimu Rasmi Imetatizwa/Si thabiti (Students with Interrupted/Inconsistent Formal Education, SIFE). Kichunguzi kinaweza kutumiwa kwa mtu binafsi au kwa kikundi na wanafunzi wanapaswa kupewa dakika zisizozidi 15 ili wakamilishe kazi. Matokeo ya kichunguzi hiki yanapaswa kutumiwa pamoja na tathmini nyingine ili kukadiria uwezo wa kuandika wa wanafunzi watarajiwa wa SIFE, ambay inaweza kuchangia kwa uamuzi wa mafunzo sahihi ya uandishi.

Kabla ya kuanza kutumia Kichunguzi, tambua lugha ya nyumbani au ya msingi kama ilivyotambuliwa kutoka kwenye Hojaji ya Lugha ya Nyumbani (Home Language Questionnaire, HLO). Kwa sasa, Kichunguzi kitolewa katika lugha zifuatazo:

- | | |
|----------------------|--------------|
| ⟨ Kiarabu | ⟨ Kinepali |
| ⟨ Kibangla | ⟨ Kirusi |
| ⟨ Kibama | ⟨ S'gawKaren |
| ⟨ Kichina | ⟨ Kisomali |
| ⟨ Kifaransa | ⟨ Kihispania |
| ⟨ Kifulani | ⟨ Kiswahili |
| ⟨ Kikrioli cha Haiti | ⟨ Kiurd |
| ⟨ MaayMaay | |

1. Ikiwa mwanafunzi ataandika kwa lugha ambayo haijaoorodheshwa hapo juu, anaweza kuandika kwa lugha hiyo akitumia kidokezo na mafunzo ya Kiingereza ambayo yametafsiriwa katika lugha yake ya nyumbani au ya msingi. Fahamu kuwa toleo la Kiingereza la Kichunguzi linapaswa kutumiwa kama chanzo cha tafsiri pekee na halipaswi kutumiwa kwa wanafunzi wa Kiingereza.
2. Mkufunzi anaweza kujaza katika sehemu ya

Jina:	Umri:
Tarehe:	Lugha ya Nyumbani:
Tarehe ya Kuwasili Marekani:	Nchi Aliyozaliwa:

Kichwa cha uandishi wako:

Kwa zoezi hili, andika kuhusu mchezo unaopenda kucheza. Tumia nafasi ifuatayo kuandika aya moja au mbili kuhusu mchezo unaopenda:

Kumbuka kujumuisha katika uandishi wako:

Jina la mchezo unaopenda
Jinsi ya kuuchenza mchezo
Maelezo kuhusu mchezo
Kumbukumbu zozote unazoweza kuwa nazo za kucheza mchezo
Sababu za kuupenda mchezo huo

	<p>Uandishi unaoeleweka na wenyе kutoa maelezo muhimu na unamshirikisha msomaji. Yanaonyesha mawazo mazito kuhusu zoezi lenyewe</p>	<p>Suala la mada linæleweka lakini linakosa maelezo. Yanaonyesha ufahamu kamili wa kazi.</p>	<p>Maelezo kidogo yatolewa, yanaweza kujumuisha maelezo yasiyo muhimu. Yanaonyesha ufahamu mchache wa zoezi lenyewe.</p>	<p>Uandishi umepotoka au una maelezo machache au hauna maelezo muhimu. Yanaonyesha ufahamu mdogo au kutolewa zoezi lenyewe.</p>
	<p>Uandishi una mshikamano na unaeleweka, wenyе mtiririko mzuri wa mawazo.</p>	<p>Uandishi unaweza kutenganishwa lakini msomaji bado anaweza kuelewa maana iliyokusudiwa. Unaweza kukosa mpangilio kiasi na/au kukuzwa kidogo.</p>	<p>Uandishi hauna mpangilio na haujakuzwa. Ni vigumu kuelewa, na mpangilio wa mawazo unazuia ufahamu.</p>	<p>Uandishi hauleti maana. Sehemu yake inaweza kuwa nakala ya kidokezo.</p>
	<p>Matumizi ya sarufi yanapanua maelezo na uandishi ni fasaha. Makosa ya tahajia hayazui ufahamu. Uzingatiaji mkubwa wa stadi za uandishi.</p>	<p>Sarufi inaweza kusababisha mkanganyiko kidogo kuhusu maana. Makosa katika stadi za uandishi na tahajia yanaweza kuzuia ufahamu.</p>	<p>Makosa mengi ya sarufi, stadi za lugha na tahajia yanazuia ufahamu.</p>	<p>Sarufi na tahajia isiyo sahihi inafanya uandishi kutofahamika. Hakuna matumizi ya stadi za uandishi yameonyeshwa.</p>
	<p>Msamiati na muundo wa sentensi zinatofautiana na ni sahihi.</p>	<p>Msamiati na muundo wa sentensi ni sahihi.</p>	<p>Msamiati na muundo wa sentensi si sahihi kwa wanafunzi. Makosa ya mara kwa mara yanazuia ufahamu.</p>	<p>Msamiati na muundo wa sentensi haufahamiki wala si sahihi. Huenda kusiwe na jibu kabisa.</p>